**Deutsche Welle**

**“Learning By Ear”**

**Mafunzo na Kazi: Muziki**

**Mwandishi: Sam Olukoya**

**Wahariri: Ulrich Neumann, Maja Dreyer**

**Tafsiri Kiswahili:Eric Ponda**

---

**1MSIMULIZI**

**1 Sauti:Mwanamuziki wa Kike miaka 28, Mlio wa Farasi**

---

**Intro**

Hujambo msikilizaji na karibu kwa mfululizo wa vipindi vyetu vya “Lern By Ear” ‘Noa Bongo Jenga maisha yako’, ambapo tunakutana na watu wenye taaluma mbali mbali. Katika kipindi cha leo tunangazia sekta ya uimbaji na tunakutana na mwanamuziki chipukizi Chimere Emejuobi kutoka Lagos, nchini Nigeria.

**1. Mazingira: Chimere akiimba**

Muziki ni muhimu sana miongoni mwa jamii nchini Naigeria. Kunauhusiano wa karibu baina ya Muziki na tamaduni za Wa-Nigeria kana kwamba Muziki ni Maisha nchini humo.Na labda hii ndio sababu kubwa ya ongezeka la idadi ya Wana Muziki nchini humo.Lakini licha ya hayo wanamuziki wengi bado wanakabiliwa na changa moto nyingi tu nchini humo.

Chimere Emejuobi ni mwanamuziki mashuhuri nchini Nigeria, lakini kwake yeye bado hii ni kama kama ndoto. Yeye ni muimbaji mashuhuri katika sekta ya filamu ambayo inaendelea kupanuka nchini humo. Na kama asemavyo “Muziki wangu unalenga kuleta sura halisi ya Bara Africa kupitia filamu tunazotayarisha katika kanda hii”.

Chimere ni mwanamuziki anayevalia nadhifu, na amepiga kambi mjini Lagos kunakoishi wengi wa wanamuziki wa nchini Nigeria.

Bila kusita anasema azma yake kuu ilikuwa kutimiza ndoto ya kuwa Mwanamuziki mashuhuri maishani.

**2. O-Ton Chimere**

Niliingia katika fani hii ya muziki nikiwa na umri wa miaka saba. Niliamua kujitosa ulimwengu wa muziki kwa kuwa naamini ninacho kipawa cha kuimba. Napenda sana kuimba na sina shaka hiki ndicho kipawa changu.

Ni kitambo kidogo akiwa bado anaishi Kusini Mashariki mwa Nigeria alipogundua kipaji chake uimbaji kwa mara ya kwanza.

**3. O-Ton Chimere**

Nilianza kuimba nikiwa mdogo katika shule ya upili, kisha nikajiunga na kwaya ya watoto kanisani, ambako niliendelea kujipa moyo kwamba naweza kuimba ..na … na niliimba! Mimi huimba sauti ya juu…. sana sana napendelea nyimbo za kigeni kama huu….em…..

**4. SFX Chimere akiimba kidogo.**

Chimere aliendelea kukuza kipaji chake punde baada ya kumaliza masomo yake ya upili.

**5. O-Ton Chimere**

Nilipomaliza masomo yangu ya shule ya sekondari nilianza kuimba pamoja na baadhi ya wanamuziki mashuhuri, kwa hiyo nikawa maarufu kama muimbaji wa kuwapokeza waimbaji wengine wakati huo, kabla kuamua kuimba peke yangu. Sasa nimetoa album ya vibao vyangu mwenyewe.

Safari yake kufikia upeo kimuziki imekumbwa na panda shuka nyingi tu. Sasa akiwa na umri wa miaka 28, Chimere, anasema, haikuwa rahisi, ikizingatiwa umri wake mdogo na ndio mwanzo alikuwa ametoka shuleni. Mbali na hayo akiwa msichana mdogo aliandamwa na malimwengu,ikiwemo kunyanyaswa kimapenzi na baadhi ya watayarishaji Muziki..

**6. O-Ton Chimere**

Wakati nilipojitosa katika fani hii ya muziki, nilifuatwa na watayarishaji wa muziki wakitaka kunirekodi vibao vyangu. Na kwa sababu sikuwa na pesa za kutosha kurekodi muziki wangu, baadhi yao walinitaka kimapenzi kabla ya kunipa nilichotaka, lakini hilo nikakataa kata kata. Nilisema siwezi kushusha hadhi yangu.

Masaibu ya Chimere yalifikia kikomo pale ndugu yake alipojitokeza kumsaidia katika kurekodi vibao vyake.

Lakini licha ya hayo bado anazungungwa na changamoto nyingi tu, kama vile wizi wa kandaa, na wauzaji wa kanda za Muziki ambao wanazidi kumgandamiza hasa kuhusu malipo,asema Chimere.

**7. O-Ton Chimere**

Wizi wa kanda za muziki unaniathiri mimi binafsi…maana hata baada ya kufanya bidii ya kuimba na kurekodi huwezi kupata malipo kwa urahisi. Kila ninapomfuata muuzaji wa muziki wangu, huniambia hakuna pesa, muziki wako haununuliwi….Hivi sasa bado nasubiri pesa zangu kutoka kwa wauzaji muziki, lakini imekuwa vigumu kupata pesa hizo.. kila wakati ni porojo tu ..leo …kesho na kadhalika. Tatizo jingine ni kunyimwa haki zangu kama mwanamuziki, sivyo nilivyotarajia.

Muziki unaochezwa sana na bendi ya Chimere's ni ule wa taratibu yaani rhythm and blues, kwa kutumia mchanganyiko wa vyombo vya muziki wa kizazi cha sasa na utamaduni wa Wa Nigeria. Miongoni mwa vifaa anavyopendelea kutumia sana Bi Chimere ni ile Zumari ya Wa Nigeria. Chombo hiki ni maarufu sana hasa miongoni mwa wakaazi wa Kusini Mashariki mwa Nigeria anakotoka Chimere.

**8. SFX Sauti ya Zumari ya Kinigeria ikitoweka chini kwa chini.**

**9. O-Ton Chimere**

Mimi hutumia sana sana vyombo vya kitamaduni kama hizi zumari. Kuna hizi zumari za kucheza nyimbo za maombolezi na zile za kawaida. Hutumia pia marimba ya kitamaduni na kamba ambazo huleta hisia. Kwa ufupi mimi hutumia vyombo vya kitamaduni kwani huleta hisia na sura ya mwafrika halisi. Mtu anapofariki na kisha ucheze vyombo hivi, si lazima mbiu.. zumari inatosha.

**8. SFX Sauti ya Zumari ya Ki-Nigeria.**

Chimere anasema zinduko lake la Muziki linatokana na msingi bora wa maisha ya ukristo katika familia yake.

**10. O-Ton Chimere**

Kinachonipa msukumo na moyo zaidi wa kuendelea na muziki ni uwezo wake mwenyezi Mungu tu. Pili ni mambo ya ulimwengu yanayotuzunguka. Kila nikitazama mambo yanayotuzunguka maishani, hushikwa na hisia na azma ya kuimba. Nyimbo ninazotunga ni kuhusu matukiko ya kawaida kila siku maishani. Ndio nyimbo zangu!

Vibao vya Chimere ni mchanganyiko wa Lugha ya Kingereza na kabila lake la Igbo.

**11. SFX Atmo: Chimere akiimba mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Igbo.**

Chimere anasema yeye hupendelea kuimba kwa lugha ya mama ili watu wasioielewa lugha ya kingereza wapate kumuelewa vyema. Na wengi wanafurahia na kupenda zaidi nyimbo zake hata Wazungu wanaotaka kujifunza lugha za Makabila mbali mbali barani Africa. Lakini sana sana Chimere hupendelea kutunga na kuandika nyimbo zinazotumika katika utayarishaji filamu.

**13. SFX Onyesho la filamu ya Nollywood.**

***Onyesho la filamu ya Ki-Nigeria*.**

Sekta ya filamu nchini Nigeria, Nollywood ni ya tatu kwa umaarufu wa utayarishaji silamu ulimwenguni baada ya ile ya Hollywood nchini Marekani na Bollywood nchini India. Filamu zinazotayarishwa na Nollywood sana sana hutilia mkazo zaidi muziki, na Chimere amefaulu kurekodi nyimbo nyingi zinazotumika katika sekta hii ya filamu nchini Nigeria..

**14. O-Ton Chimere**

Sababu iliyopelekea mimi kujiingiza katika uimbaji wa muziki unaotumiwa kwa utayarishaji filamu za Nollywood ni kwamba, nilitaka kutambuliwa kama mtumbuizaji maarufu, na kuchukua nafasi yangu inayostahiki katika sekta hiyo. Sasa nimegundua kuna muziki maalumu unaotumiwa katika filamu.

Chimere alitunga wimbo wake wa kwanza ujliotumika katika filamu za Nigeria akiwa bado Shule ya upili

Anasema mwanzoni haikuwa rahisi kwasababu watayarishaji Muziki walimudharau kuwa si Mtu mwenye ujuzi wa kutosha katika fani hiyo, na kwa hiyo wakawa na kusitasita kujihusisha naye kimuziki.

**15. O-Ton Chimere**

Nilijaribu kuwasihi wadhamini wakuu wa utayarishaji filamu nchini Nigeria, kwamba naweza kutunga na kuimba nyimbo zinazoweza kuzua hisia na hata kuiga hisia… lakini wapi! Ilinichukua muda mrefu kuwashawishi wanikubali. Nilipokuwa katika shule ya sekondari nilitunga wimbo mmoja na baada ya kumaliza masomo nikaanza kutunga na kutayarisha nyimbo hizi…ni nyingi.

| **13. SFX Onyesho la Filamu ya Ki-Nigeria,Nollywood** |
|---|

Chimere anasema kuwa kunauhusiano mkubwa baina ya Muziki wake na Filamu za Wa-Nigeria kwa kuwa hutayarishwa kwa misingi na dhamira ya kutoa sura halisi ya Africa.

| **16. O-Ton Chimere** |
|---|
| Sana sana mimi hutumia muziki wangu kuongeza ladha katika filamu hizi za Nigeria, nyingi zikiwa ni za utendi, zinazohitaji zaidi muziki wa Kiafrica. Mimi hutumia muziki kama chombo cha kuelezea yanayojiri kwenye hadithi ya filamu ili iweze kueleweka kwa ufasaha zaidi, na pia kuleta ile sura halisi ya filamu za Kiafrika. |

**Outro:**

Kwa kutafakari miaka inavyokwenda,Chimere anaridhika na taaluma au kipawa chake. Na kinachomvutia zaidi ni jinsi Muziki ulivyombadili kutoka mwana kwaya kanisani hadi kufikia upeo wa Muziki mashuhuri nchini Nigeria.

Haikuwa rahisi kufika nilipo sasa, lakini kama muonavyo, kutokana na bidii, hakuna lisilowezekana ila tuj Mtu anapasa kupewa motisha kutimiza ndoto yake. Iwapo unataka kujifahamisha zaidi kuhusu kazi au taaluma tembelea ukurasa wa mtandao wetu www.dw-world.de/lbe. na pia unaweza kusikiliza vipindi vyetu vya Lerning by Ear, Noa bongo jenga Maisha yako. Ni hayo tu kwa leo hadi wakati mwengine Kwaheri